# SWAHABA NA MAMA WA WAUMINI

## KWA NINI TUNAWAPENDA NA KUWATETEA?

**MWANDISHI**

**Ally Abdallah Al-ammaary**

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila sifa njema anazistahiki Allah, na rehema na amani ziwe juu ya Mtume wetu na Kiongozi wetu, Muhammaad Bin Abdallah, pamoja na Familia yake na Swahaba wake.

Ama baada ya hayo:

Baadhi ya watu wanauliza: Kwa nini tunawapenda Swahaba na mama wa waumini? Kwa nini tunawapenda na kuwatetea?

Kabla ya kujibu ni vizuri tumtambulishe Swahaba.

**Swahaba ni mtu ambaye alikutana na Mtume (s.a.w.) katika uhai wake akiwa Muislamu na akafa akiwa katika Uislamu wake**. [Al-iswaabah Fii Tamyiiz Swahabah 1/8].

**Na ni nani mama wa Waumini?** Mama wa Waumini ni wake wa Mtume (s.a.w). Allah amewasifu wake wa Mtume kwamba ni mama wa Waumini. Allah amesema kuwa: ***"Nabii (Muhammad) ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao na wake zake ni mama zao".*** [Sura Al-ahzaab, aya 6].

Wake wa Mtume ni Khadija Bint Khuwailid, Sawdah Bint Zamah, Aisha Bint Abubakar Swiddiiq Attaymiyyah, Hafswa Bint Umar Binkhatwaab Al-adawiyyah, Zainab Bint Khuzaimah Alhilaaliyyah, Ummusalamah ambaye jina lake ni Hindu Bint Abu-umayyah Bin Mughiirah Almakhzuumiyyah, Zainabu Bint Jahsh Al-asadiyyah, Juwairiyyah Bint Haarith Alkhuzaaiyyah, Rayhaana Bint Zaid Bin Amru Alquradhwiyyah, Ummuhabiba ambaye jina lake ni Ramlah Bint Abusufiyan Al-umawiyyah, Swafiyyah Bint Huyayy Bin Akhtwab Annudhwairiyah, Maimuna Bint Harith Bin Huzni Alhilaaliyyah. Mtume (s.a.w.) alifariki akicha wake (wajane) tisa miongoni mwa wake zake wote. Wajane hao ni Sauda, Aisha, Hafswa, Ummusalam, Zainab Bint Jahshi, Ummuhabiba, Juwairiya, Swafiya na Maimuna. Tunaomba radhi za Allah ziwafikie wote.

Kwa kurejea kwenye jawabu la swali ni kwamba, kuwapenda Swahaba na Mama wa Waumini ni itikadi iliyokubalika kwa Ahlusuna Waljamaa (Suni).

Allah amewasifia Swahaba wa Mtume (s.a.w.) katika sehemu nyingi ndani Qur-ani Tukufu. Allah Mtukufu amesema kuwa: "***Yeye ndiye aliyekutia nguvu kwa nusura yake na kwa Waumini, Na akaunganisha baina ya nyoyo zao. Na lau kama wewe ungetoa vyote***

***vilivyomo duniani usingeweza kuunganisha baina ya nyoyo zao, lakini Allah ameunganisha baina yao. Hakika, yeye ni Mwenye nguvu kubwa, Mwenye hekima".*** [Sura Al-anfaal, aya 62-63].

Pia Allah Mtukufu amesema kuwa: "***Ewe Nabii, Allah anakutosheleza wewe na waumini walio kufuata".*** [Sura Al-anfaal, aya 64].

Amesema Allah Mtukufu kuwa: "***Hakika, wale walio amini na wakahama na wakapigana Jihadi katika njia ya Allah kwa mali zao na nafsi zao, na wale walio toa hifadhi (mahala pa kukaa), na wakatoa nusura (msaada kwa ndugu zao), hao, baadhi yao ni marafiki na walinzi wao kwa wao".*** [Sura Al-anfaal, aya 72].

Pia amesema Allah Mtukufu kuwa: "***Wale walio amini, na wakahama, na wakapigana Jihadi katika njia ya Allah kwa mali zao na nafsi zao, hao wana hadhi kubwa zaidi mbele ya Allah. Na hao ndio wenye kufuzu. Mola wao anawapa habari njema ya kupata rehema zitokazo kwake, na radhi, na bustani ambazo humo watapata neema za kudumu. Watadumu humo milele. Hakika, kwa Allah yapo malipo makubwa".*** [Sura Attawbah, aya 20 - 22].

Na amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Na wale walio tangulia, wa mwanzo, katika Muhajirina na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Allah ameridhika nao, na wao wameridhika naye, na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wakae humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa".*** [Sura Attawba, aya 100].

Allah Mtukufu amesema kuwa: ***"Kwa hakika kabisa, Allah amewaridhia waumini pale walipokula kiapo cha utiifu kwako chini ya mti, akajua yaliyomo nyoyoni mwao, basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa ushindi wa karibu".*** [Sura Alfat-hi, aya 18]. *Sheikhul-islam Ibnitaimiya, rehema za Allah zimfikie, amesema kuwa:* ***"Kuridhiwa na Allah ni sifa kongwe. Allah hawi radhi na mja isipokuwa tu yule ambaye amejua kwamba atamkabili kwa kutekeleza mambo yanayowajibisha kupata radhi. Mtu ambaye Allah amemridhia kamwe hawezi kumkasirikia .*** [Asswwaarimul-masluul Alaa Shaatimirrasuul, Uk. 572].

Na amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Muhammad ni Mtume wa Allah, na waliopo pamoja naye ni wenye nguvu mbele ya makafiri, wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakirukuu, wakisujudu wakitafuta fadhila na radhi za Allah. Alama zao zipo katika nyuso zao kutokana na athari ya kusujudu. Huo ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili ni kama mmea ulio toa chipukizi lake, likautia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya jiti lake, ukawafurahisha wakulima, ili kwa ajili yao awakasirishe makafiri. Allah amewaahidi walio amini na wakatenda mema miongoni mwao msamaha na ujira mkubwa"*** . [Sura Alfat-hi, aya 29].

Na amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa (mali na nafsi zao) kabla ya ukombozi (wa mji wa Makka) na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko***

***wale walio toa baadae na kupigana vita. Na wote hao Allah amewaahidi mazuri".*** Sura Alhadiid, aya 10.

Na amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Wapewe fukara wahamiaji waliotolewa majumbani mwao na (kunyan'ganywa) mali zao wakitafuta fadhila za Allah na radhi (zake), na wakimnusuru Allah na Mtume wake. Hao ndio wakweli (katika Uislamu wao)".*** Sura Alhashri, aya 8.

Amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Siku ambayo Allah hatamfedhehesha Nabii na wale walio amini pamoja naye. Nuru yao inatembea mbele yao na pande zao za kulia, wakisema: Ewe Mola wetu, tutimilizie nuru yetu, na utusamehe. Hakika, wewe ni Mwenye uwezo wa kila kitu".*** Sura Attahriim, aya 8.

Ama katika Hadithi, imenukuliwa kwa Abuhuraira, radhi za Allah zimuendee, akisema kuwa, amesema Mjumbe wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake, kwamba: "***Msiwatukane Swahaba wangu, msiwatukane Swahaba wangu. Nina apa kwa (jina la Allah) ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake kwamba, lau kama mmoja wenu angetoa dhahabu mfano wa mlima wa Uhud (kwa ajili ya sadaka au kuendeleza dini), asingefikia kibaba cha mmoja wao au nusu yake".*** Hadithi hii imepokewa na Imam Muslim.

Na katika Sahih Muslim na Sahih Bukhari imethibiti kunukuliwa kwa Abdallah Ibnimasoud, radhi za Allah zimwendee, akisema kuwa, Mtume (s.a.w.) amesema kwamba: ***"Watu bora zaidi ni karne yangu, kisha ni wale wanaowafuatia, kisha ni wale wanaowafuatia".***

Na imenukuliwa kwa Abubarda, radhi za Allah zimuendee, akisema kuwa, amesema Mjumbe wa Allah, rehema na amani zimfikie, kwamba: ***"Nyota ni mlinzi wa (usalama wa) mbingu. Nyota zikiondoka, yataifika mbingu yale iliyoahidiwa (kupasuka kwa mbingu na kuporomoka kuashiria Kiama). Na mimi ni mlinzi wa (usalama wa) Swahaba wangu. Nikiondoka, yatawafika Swahaba wangu yale wanayoahidiwa (Kutokea kwa misukosuko, ugonvi na kupigana). Na Swahaba wangu ni walinzi wa (wa usalama wa) uma wangu. Swahaba wangu wakiondoka, yataufika uma wangu yale wanayo ahidiwa (Kutokea kwa Bidaa na uzushi katika dini na matukio mengi mabaya katika dini)".*** Hadithi hii imepokewa na Imam Muslim.

Na imenukuliwa kwa Abdallah Bin Mughaffal Almuzaniy akisema kuwa, amesema Mjumbe wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake, kwamba: ***"(Muogopeni) Allah (Muogopeni) Allah kwa Swahaba wangu. Msiwavunjie heshima baada yangu. Atakaewapenda, ni kwa kunipenda mimi ndio maana amewapenda, na atakayewachukia, ni kwa kunichukia mimi ndio maana amewachukia. Na atakaye waudhi, hakika ameniudhi mimi, na atakaye niudhi mimi hakika amemuudhi Allah. Na atakayemuudhi Allah inakaribia kwake kumchukulia hatua kali (kwa kumuadhibu)".*** Hadithi hii imepokewa na Imam Tirmidhiy.

Na amesema Mtume (s.a.w.) kamba: ***"Mwenye kuwatukana Swahaba wangu, basi laana ya Allah na Malaika wake na watu wote imshukie".*** Ameipokea Hadithi hii imam Twabaraaniy. Sheikh Al-albaniy katika kitabu chake cha Silsilat Hadiith Sahiha 5/446 ameitaja hii kwamba ni Hadithi "Hasan".

Na katika Sahih Bukhari na Sahih Muslim imethibiti kunukuliwa kwa Baraa Bin Aazib kwamba, Mtume (s.a.w.) aliwaelezea Answaar (Swahaba wenyeji wa mji wa Madina) kwa kusema kuwa: ***"Hatawapenda isipokuwa tu muumini, na hatawachukia isipokuwa tu mnafiki. Atakaye wapenda, Allah atampenda, na atakaye wachukia Allah atamchukia".***

Na amesema Ibnimasoud, radhi za Allah zimfikie, kwamba: ***"Hakika, Allah aliangalia nyoyo za waja akakuta moyo wa Muhammad (s.a.w.) ni moyo bora zaidi kati ya nyoyo za waja na, kwa sababu hiyo, akamteua kwa ajili yake na kumtuma kufikisha ujumbe wake. Kisha Allah aliangalia nyoyo za waja baada ya moyo wa Muhammad akakuta nyoyo za Swahaba wake ni nyoyo bora zaidi kati ya nyoyo za waja na,kwa sababu hiyo, akawafanya wasaidizi wa Mtume wake ; wanaopigana kwa ajili ya dini yake".*** Hadithi hii imepokewa na Imam Ahmad.

Na imenukuliwa kwa Abdallah Bin Omar, radhi za Allah zimuendee yeye na baba yake, akisema kwamba: ***"Mwenye kutaka kuiga, awaige (wale) waliokwishakufa. Hao ni Swahaba wa Mtume (s.a.w.). Walikuwa na mioyo mema sana, elimu iliyozama ndani sana, wachache wa kujibebesha magumu. Ni watu ambao Allah aliwachagua ili kusuhubiana na Mtume wake (s.a.w.) na kubeba dini yake. Igeni tabia na mienendo yao, kwa sababu wao, ni Swahaba wa Muhammad (s.a.w. na) walikuwa katika mwongozo wenye kunyooka".*** Ameipokea Hadithi hii Abunuaim katika kitabu chake cha Al-hilyah 1/305-306.

Anasema Kadhi Ibnuabil-izzi Addimashqiy katika kitabu chake cha Al-aqiida Attwahaawiyyah 2/689 akiwaelezea Swahaba kwamba: ***"Na tunawapenda Swahaba wa Mjumbe wa Allah. Hatuvuki mipaka katika kumpenda yeyote miongoni mwao na hatumtengi yeyote miongoni mwao. Tunamchukia anayewachukia na kuwasema vibaya. Hatuwataji isipokuwa kwa kheri tu. Kuwapenda ni dini, ni imani na ni jambo zuri. Kuwachukia ni ukafiri, ni unafiki na ni kuvuka mipaka".***

*** SWAHABA WOTE NI WAADILIFU NA HAIFAI KUHOJI UADILIFU WAO:**

Amesema Imam Nawawiy kwamba: ***"Swahaba wote ni waadilifu; waliokumbana na mitihani na wasiokumbana nayo, kwa mujibu wa makubaliano ya wale (wanazuoni) wanaokubalika".*** Attaqriib, Uk. 214.

Amesema Ibniswalaah kwamba: ***"Uma umekubaliana juu ya uadilifu wa Swahaba wote, na hata wale waliokumbana na mitihani miongoni mwao".*** Alhadiith Walmuhaddithuun, Uk. 129/130.

Amesema Alkhatwiib Albaghdaadi kwamba: ***"Haya ni maelezo ya jinsi Allah na Mtume wake walivyo taja uadilifu wa Swahaba, na kwamba hakuna haja ya kuhoji uadilifu wao, isipokuwa tu ni wajibu kuhoji uadilifu wa walio chini ya hadhi yao".*** Alkifaaya, Uk. 46.

## HAIFAI KUMTUKANA SWAHABA YEYOTE AU KUMKEJELI:

Amesema Sheikhul-islam Ibnitaimiyah, Allah amrehemu, katika kuelezea lililo wajibu kuhusu Swahaba wa Mjumbe wa Allah kwamba: ***"Katika misingi ya Ahlusun Waljamaa (Suni) ni mioyo na ndimi zao kuwa salama kwa Swahaba wa Allah, kama Allah alivyo wasifia katika kauli yake isemayo kuwa: "Na walio kuja baada yao (Swahaba) wanasema: Ewe Mola wetu: Tusamehe sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa imani, na usiweke ndani ya nyoyo zetu mfundo (chuki) kwa walio amini. Ewe Mola wetu, hakika wewe ni Mpole sana, Mwenye kurehemu"***. Sura Alhashri, aya 10. [Sharhul-aqiidatil-waasitwiyyah, Uk. 184].

Amesema Ibniabbas, radhi za Allah zimfike yeye na baba yake, kwamba: ***"Allah ameamrisha kuwaombea msamaha Swahaba wa Muhammad huku akijua kwamba watakuja kupigana".*** [Sheikhul-islam Ibnitaimiyah, Asswaarimulmasluul, Uk. 584].

Amenukuliwa Ibniomar, radhi za Allah zimfikie yeye na baba yake, akisema kwamba: ***"Msiwatukane Swahaba wa Muhammad, kwa sababu kisimamo cha mmoja wao (katika kusali) muda mdogo tu ni bora zaidi kuliko ibada za mmoja wenu umri wake wote"***. [Ameipokea Ibnnimaajah na Ibniabii Aaswim katika Sunnah, na nukuu yake ni sahihi].

Mama wa Waumini, Aisha, radhi za Allah zimfikie, aliambiwa kuwa, kuna watu wanawasema vibaya Swahaba wa Mtume wa Allah (s.a.w.) mpaka Abubakar na Omar, radhi za Allah ziwaendee, akasema kuwa: ***"Mnayashangaa haya? Ibada zao zimeshawakatikia. Kwa hiyo, Allah amependa thawabu zisiwakatikie"***. [Sheikhul-islam Ibnitaimiyah, Minhaajussunsa Annabawiyyah, 1/22].

Amesema Imam Maalik, rehema za Allah zimuendee, kwamba: ***"Mwenye kumtukana Swahaba yeyote wa Mtume (s.a.w.) na Abubakar, Omar, Othman, Ally Muawiya au Amr Ibnil-aasw; akisema kuwa Swahaba hao walikuwa katika upotevu na ukafiri, ni kwamba atauliwa. Ikiwa amewatukana kama wanavyotukana watu, tofauti na matusi haya (ya upotovu na ukafiri), ataadhibiwa adhabu kali sana".*** [Alqaadhwi Iyaadh, Alshifaa Fii Huquuqilmustwafaa, Uk. 299].

Imenukuliwa kwa Abubakar Almarwaziy akisema kuwa: ***"Nilimuuliza Abuabdallah kuhusu mtu anayemtukana Abubakar, Omar na Aisha, akasema kwamba: Sioni kama yumo katika Uislamu".***

[Alkhallaal, Assunnah: 3/493].

Amesema Abuzur-a Arraaziy kwamba: ***"Ukimuona mtu anamkejeli***

***Swahaba yeyote wa Mtume wa Allah, tambua kuwa huyo ni mzandiki".*** [Alkifaayah Fii Ilmirriwaayah, Uk. 97].

Amesema Imam Ahmad, rehema za Allah zimuendee, kwamba: ***"Ukimuona mtu anawataja Swahaba wa Mtume wa Allah kwa ubaya mtilie shaka juu ya Uislamu wake".*** [Allaalakaalii, Sharhu Usuulul-iitiqaad: 7/ 1252].

## NI KATIKA HAKI ZA SWAHABA KUUNYAMAZIA UGONVI ULIOTOKEA BAINA YAO:

Madhehebu ya Ahlusuna Waljamaa (Suni) ni kuunyamazia ugonvi uliotokea kati ya Swahaba, radhi za Allah ziwe yao. Yule mwenye kupatia (katika ugonvi huo) ana malipo ya aina mbili, na yule mwenye kukosea ana malipo ya aina moja tu.

Kumbuka ewe Muisalmu kwamba, Siku ya Kiama Allah atakuu-liza kuhusu matendo yako ***"Kila nafsi itafungika kwa ilicho kichuma".*** Sura Almuddath-thir, aya 38. Allah hatakuuliza kuhusu matendo ya watu wengine wakiwemo waliokwisha pita. Hatakuuliza kwamba, nani alikuwa na haki? Nani alikosea na nani alipatia? Amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Hao ni watu waliokwisha pita. Watapata waliyo yachuma, nanyi mtapata mliyo yachuma, na hamtaulizwa kuhusu waliyokuwa wakiyafanya".*** Sura Albaqarah, aya 134.

Huyu hapa Omar Bin Abdulaziz, rehema za Allah zimuendee, kama ilivyonukuliwa katika kitabu cha Aljaamiu li-ahkaamil-qur-ani cha Qurtubiy 16/122, alipoulizwa kuhusu vita vilivyotokea kati ya Ally na Muawiyah alisema kwamba: ***"Hizo ni damu (ambazo) Allah ameisafisha mikono yangu isihusike kuimwaga, kwanini nisiusafishe ulimi wangu (uache kuwaseme vibaya)?.*** Kisha akasema kwamba: **"*Mfano wa Swahaba wa Mtume wa Allah ni mfano wa macho. Dawa ya macho ni kuacha kuyagusa".***

Aulizwa Imam Ahmadi Bin Hambal, rehema za Allah ziwe juu yake, kama ilivyonukuliwa katika kitabu cha Assunnah cha Alkhal-laal 2/460 kwamba: ***"Unasemaje kuhusu hali (ya ugonvi) iliyopo kwa Ally na Muawiya, rehema za Allah ziwaendee? Alisema: Sisemi kuwahusu wao isipokuwa mazuri tu. Namuomba Allah awarehemu wote".***

Haya hayapingani na vitabu vilivyoandikwa na Ahlusuna (Suni) vikizungumzia yaliojiri kati ya Swahaba na kuyatolea muelekeo sahihi na pia kujibu tuhuma za wapotoshaji.

## NINI HUKUMU YA KUWATUKANA MAMA WA WAUMI-NI AU KUWAVUNJIA HESHIMA ?

Hapana shaka kwamba, kuwalaani wake wa Mtume (s.a.w.) ni tuhuma nzito na ni dhambi kubwa. Amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Hakika, wale wanao muudhi Alla na Mtume wake, Allah amewalaani***

***duniani na Akhera, na amewaandalia adhabu ya kufedhehesha".*** Sura Al-ahzaab, aya 57.

Mtume (s.a.w.) amenukuliwa akimuelezea Aisha kwamba: ***"Msiniudhi kwa Aisha".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Kuhusu hukumu ya anayewatusi wake wa Mtume (s.a.w.), amesema Kadhi Abuyaalaa kwamba: ***"Mwenye kumtuhumu Aisha kwa tuhuma ambazo Allah alimsafisha atakuwa kafiri, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni wote. Wanazuoni zaidi ya mmoja wamenukuu makubaliano haya na pia maimamu zaidi ya mmoja wametamka wazi hukumu hii (ya kuuawa kwa anayemtuhumu Aisha kwa uzinifu)".*** [Asswaarimulmasluul Alaa Shaatimirrasuul, Uk. 565-566].

Kadhi Iyadh amemnukuu Imam Malik, rehema za Allah zimuendee, akisema kuwa: ***"Mwenye kumtukana Aisha anauawa. Aliulizwa: Kwa nini? Alisema: Mwenye kumtupia Aisha tuhuma (za uzinifu) hakika ametofautiana na Qur-ani".*** Ibnishaban akimnukuu Imam Malik amesma kuwa: ***"Ni kwa sababu Allah anasema kuwa: [Allah anakuonyeni msirejee tena (kusema) kama hayo kabisa, ikiwa nyinyi ni Waislamu wa kweli].*** Sura Annur: 17***. Mwenye kurudia (kusema) mfano wake atakuwa amekufuru".*** Asshifaa Fii Huquuqilmustwafaa, Uk. 299.

Kila Muislamu atambue kwamba, ubora wa mtu kuwa swahaba umethibiti kwa Swahaba wote ambao wameingia katika utambulisho uliotangulia na ambao umekubalika kwa Ahlusuna. Ni ujinga mbaya sana unaoenezwa na wazushi wa sasa kuifunga maana ya Swahaba katika kikundi cha wachache na kuwaacha Swahaba wengine. Yote hayo ni muendelezo wa pumzi chafu za Shia zinazo wachukia Swahaba kwa kujenga hoja ya kuwatoa wengi katika uswahaba.

Mwanachuoni wa Hadithi Shekh Suleiman Al-alwani katika kitabu chake cha Al-istinfaar lidh-dhabbi Anisw-swahaaba Al-akhyaar Uk. 20 anasema kwamba: ***"Badhi ya watu wa wanaopenda kufuata utashi wao binafsi wamedai kwamba, uswahaba haupatikani isipokuwa tu kwa Muhaajirina na Answaar. Kwa maana hiyo, hauithibiti uadilifu wa waliokuja baada yao isipokuwa tu kwa yale ambayo kwayo umethibiti uadilifu wa wengine, wakiwemo Taabiina na wengineo. Hili ni kosa ambalo halijasemwa na Ahlisuna yeyote".*** Mwisho wa kunukuu.

Pia ni dhambi kumsema kwa ubaya Muawiya Bin Abisufian kwa hoja kwamba: a) Alipigana na Ally Bin Abitwalib, au kwamba: b) Aliingia katika Uislamu mwaka wa [fat-hu = mwaka ulipokombolewa mji wa Makka] au kwamba: c) Aliritadi (alitoka katika Uislamu) baada ya vita vya Hunain! Yote hayo hayafai. Hakuna mwanachuoni yeyote aliyesema kwamba Muawiya aliritadi na kutoka katika Uislamu baada ya vita vya Hunaini. Waislamu wamekubaliana kwamba Muawiya Bin Abisufian ni Swahaba bora, ni mkweli katika Uislamu

wake na uaminifu wake. Muawiya alishiriki katika vita vya Hunaini. Allah amemsafisha Muawiya pamoja na Swahaba wengine katika Qur'ani. Allah Mtukufu amesema kuwa: ***"Hakika, Allah amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunaini ambapo wingi wenu ulikupeni kiburi na, kwa sababu hiyo, haukukusaidieni kitu. Na ardhi ikawa finyu kwenu pamoja na upana wake. Kisha mkageuka na kurudi nyuma. Kisha Allah akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya waumini, na akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale walio kufuru. Na hayo ndio malipo ya makafiri".*** Sura Attawbah, aya 25 - 26. Muawiyah alikuwa miongoni mwa waumini ambao Allah amewateremshia utulivu. Sasa vipi atoke katika dini baada ya hapo, ilhali Allah amemteremshia utulivu?

Amesema Allah Mtukufu kuwa: ***"Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa (mali na nafsi zao) kabla ya ukombozi (wa mji wa Makka) na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale walio toa (mali na nafsi zao) baadae na kupigana vita. Na wote hao Allah amewaahidi mazuri na Allah anayajua mnayoyatenda".*** Sura Alhadiid, aya 10.

Muawiya ni miongoni mwa walioahidiwa mazuri na Allah. Alitoa mali yake katika vita vya Hunain na Twaif na alishiriki kupigana katika vita hivyo.

Kwa nukuu sahihi imethibiti Hadithi ya Abdulrahman Bin Umairah katika Sunan Attirmidhy kwamba, Mtume (s.a.w.) alimuombea dua Muawiya kwa kusema kuwa: ***"Allahumma Ij-alhu Haadiyan Mahdiyyah Wahdi Bih = Ewe Mola wangu, mfanye (Muawiya) kiongozi, muongofu na ongoza kwaye".***

Imethibiti katika kitabu cha Albidaayah Wannihaayah cha Ibnikathiir 8/134 kwamba Omar Bin Khatwaab, radhi za Allah zimuendee, alipompa Muawia uongozi wa Sham alisema kuwa: ***"Msimtaje Muawiya isipokuwa tu kwa kheri".*** Pia katika kitabu hicho hicho 8/134 imethibiti kunukulia kwa Ally Bin Abitwaalib, radhi za Allah zimuendee, akisema baada ya kurejea katika vita vya Swaffaini kwamba: ***"Enyi watu, msiuchukie uongozi wa Muawiya, kwa sababu mkimpoteza mtaona vichwa vinapukutika mabegani (na kuzagaa ardhini) kama vile maboga pori (yatatokea machafuko na watu kuuana kwa kukatana vichwa na vichwa hivyo kuzagaa kama maboga)".***

Katika Sahih Bukhari [Mlango wa Fadhwaail Swahaabah, Fasili ya Dhikru Muawiya] imenukuliwa kwamba, Ibniabbas aliulizwa hivi: ***"Je, una lolote la kusema kuhusu kiongozi wa Waislamu, Muawiya? Kwa sababu, hasali sala ya Witiri isipokuwa rakaa moja tu? (Ibniabbas) Alisema kuwa: Yeye (Muawiya) ni mwanachuoni".***

Katika kitabu cha Assunnah cha Alkhallaal 1/444 amenukuliwa Imam Azzuhriy akisema kuwa: ***"Muawiya (katika uongozi wake)***

***alitekeleza sera za Omar Bin Khatwaab kwa miaka mingi bila ya kuvunja chochote katika sera hizo".***

Ibniqudama Almaqdisiy katika kitabu chake cha Lum-atul-iitiqaad Alhaadiy Ilaa Sabiilirrashaadi, Uk. 33 anasema kuwa: ***"Muawiya ni mjomba wa Waumini, Mwandishi wa Wahyi (Ufunuo) wa Allah na mmoja wa Makhalifa (viongozi) wa Waislamu, radhi za Allah ziwaendee"***.

Mwanachuoni wa Hadithi Shekh Sulaiman Al-alawan katika kitabu chake cha Al-istinfaar Lidh-dhabbi Anisswahaaba Al-akhyaar, aki-muelezea Muawiya Bin Abisufian, anasema kuwa: ***"Mwenye kumpa Muawiya sifa ya unafiki baada ya kukiri kuwa ni muumini, atakuwa amejibebesha uzushi na madhambi makubwa. Mtu kama huyu ni wajibu kumtaka atubu. Akikubali kutubu na kurudi kwa Mola wake, ataseme-hewa. Akikataa kutubu, ni wajibu kwa kiongozi kumuua, kwa mujibu wa kauli sahihi zaidi kati ya kauli mbili za wanazuoni".***

Na amesema Alrabii Bin Naafii Alhalabiy [Aliyefariki mwaka 241 Hijiria] amesema kuwa: ***"Muawiya ni pazia kwa Swahaba wa Muhammad (s.a.w.). Mtu anapolifunua pazia anakuwa amejipa ujasiri wa kuchun-gulia yale yaliyopo nyuma ya pazia hilo".*** [Albidaayah Wannihaayah 8/139].

Ewe Muislamu unayewapenda Swahaba wa Mtume (s.a.w.) na unayewapenda wake za Mtume walio wasafi na wenye kujiheshimu, kumbuka kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa: ***"Na waliokuja baada yao wanasema: Ewe Mola wetu, tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa imani".*** Sura Alhashri, ay 10.

Wewe kuwa hivyo. Waombee radhi na waombee rehma wale ambao Allah amewapa heshima ya kuishi na Mtume duniani na kuwa pamoja naye peponi.

Epuka kufuata njia ya waliofedheheshwa na kupingana na njia ya Mola wa walimwengu na muongozo wa Bwana wa Mitume (s.a.w.).

Kumbuka, ewe Muislamu kwamba, Swahaba na mama wa Waumini walikuwa katika dini tukufu iliyonyooka. Katika nafsi zao walibeba upendo, kheri na uaminifu. ***"Muumini tu ndiye anayewapenda na mnafiki tu ndiye anayewachukia. Anayewapenda, Allah naye anampenda na anayewachukia Allah naye anamchukia"***. [Muswannaf Ibni Abishaiba 7/541].

Rehema na amani za Allah zimuendee Nabii Mteule, Swahaba wake wema, wake zake wasafi na wote wenye kufuata muongozo wao mpaka Siku ya Kiama.

Wassalaam alaikum warahmatullah wabarakaatuh

**Alfajiri ya siku ya Ijumaa**
**21/Jumada l-uulaa/1433**

**Mtunzi: Ally Bin Abdallah Bin Abdallah Bin Muhammad Al-ammary**